# Mifugo 18,102, kaya 677 zahamishwa Ngorongoro

**Na Ikunda Erick, Handeni**

SERIKALI imesema hadi sasa mifugo 18,102 ya kaya 677 imehamishwa kutoka ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro mkoani Arusha.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi amesema kaya hizo zenye watu 3,822 zimehama kwa hiari kutoka Ngorongoro kwenda katika Kijiji cha Msomera wilayani Handeni mkoani Tanga na maeneo mengine.

Matinyi alisema hayo alipozungumza na waandishi wa habari jana katika eneo la mradi wa makazi, malisho na kilimo katika Kijiji cha Msomera.

"Kesho (leo) kaya nyingine 72 zenye watu 515 zinahamia hapa Msomera na bado zoezi la kuwahamisha linaendelea kadri ujenzi wa nyumba unapokamilika," alisema.

Matinyi alisema katika awamu ya pili iliyoanza mwaka jana hadi Januari 12, mwaka huu kaya 525 zimejiandikisha kuhama na 126 tayari zimehamia Msomera na maeneo mengine zikiwa na mifugo 2,581.

Alisema kaya 74 kati ya hizo zenye mifugo 1,599 zimehamia Msomera na kaya nyingine 52 zenye watu 292 na mifugo 982 zimehamia maeneo ambayo wananchi hao wameyachagua.

Matinyi alisema serikali imeendelea kuboresha miundombinu katika eneo la Msomera na kilometa 150 za barabara zimekamilika ujenzi kati ya kilomita 800 zilizopangwa kujengwa.

Aidha, alisema visima vya maji 10 vimechimbwa, usambazaji wa umeme unaendelea, ujenzi wa shule ya msingi umekamilika, wa sekondari unaendelea ikiwa na maabara ya kisasa.

Alisema ujenzi wa vituo vya kuuzia maziwa unaendelea, ujenzi wa majosho na minara ya mawasiliano ya simu ipo na mingine inaendelea pamoja na upimaji wa viwanja.

Matinyi alisema awamu ya pili ya kuwahamisha wakazi hao itaendelea hadi mwishoni mwa Machi mwaka huu na katika awamu nyingine utazingatia mafanikio ya kazi inayoendelea sasa.

Alisema kaya zinazohama Ngorongoro kwa hiari zinalipwa fidia ya mali yakiwamo maboma yanayobomolewa, zinapewa shilingi milioni 10, nyumba yenye sebule na vyumba vitatu vya kulala na chakula cha miezi 18.

Aidha, alisema gharama za ujenzi wa nyumba hizo inakadiriwa kuwa kati ya shilingi milioni 15 hadi 25 kutegemea na wakati na gharama za vifaa.

**Akemea upotoshaji**

Matinyi alisema upotoshwaji unaofanywa na wanaharakati na vyombo vya habari vya kigeni unatokana na makundi hayo kutofahamu hali halisi ya maeneo hayo.

"Wapo wanaopotosha kwa kudhamiria kuitoa fahari ya Ngorongoro yenye hadhi nne za kimataifa katika dunia, tunawasihi hawa waje Tanzania wakajionee kwa macho na kupata ukweli wa Ngorongoro na Msomera, hakuna uvunjaji wa haki za binadamu," alisema.

Matinyi alisema shughuli za binadamu na mifugo vimeathiri uhifadhi katika eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 3,700 kati ya 8,000 za hifadhi hiyo ambazo ni sawa na asilimia 40 ya eneo lote.

"Hali hii ya uharibifu ikiendelea itaathiri shughuli za uhifadhi na wataalamu walifanya utafiti na kubaini katika eneo hilo ambalo wananchi na mifugo ipo, imeleta mimea vamizi ambavyo ni hatari kwa ekolojia ya hifadhini lakini pia ifikapo mwaka 2060, kama hatua madhubuti hazitachukuliwa kuilinda hifadhi hii inaweza kutoweka na wanyama wakahama," alisema.

Awali waandishi wa habari walitembelea hifadhi hiyo kuona hali halisi na kubaini makundi makubwa ya mifugo yametapakaa katika kata za Nainokanoa na Alailelai.


Katika Kijiji cha Msomera maisha ya wananchi waliohamia hapo yanaendelea kuboreka.

Wanahabari walishuhudia kaya zimelima mahindi na yameshakomaa, huduma za kijamii zikiendelea kutolewa zikiwamo shule, kituo cha afya, maji, mawasiliano na miundombinu ya barabara.

Diwani wa Kata ya Kakesio - Ngorongoro aliyehamia Msomera, Johannes Tiamas aliishukuru serikali kwa kuboresha maisha yao.

"Hapa Msomera tuna uhuru wa kufanya kazi za maendeleo na tuko salama dhidi ya wanyama wakali, hapa tunafuga na kulima, tunapata chakula cha kutosha," alisema Tiamas.

Mkazi wa Msomera kutoka Ngorongoro, Ole Mingati alisema kwa miaka mingi alikuwa kifungoni katika hifadhi ya Ngorongoro lakini sasa yuko huru ndani ya Msomera.



**katika awamu ya pili iliyoanza mwaka jana hadi Januari 12, mwaka huu kaya 525 zimejiandikisha kuhama na 126 tayari zimehamia Msomera na maeneo mengine zikiwa na mifugo 2,581.**

# Wafugaji, hifadhi wamaliza mzozo mifugo 800 yaachiwa

Joseph Lyimo, Mwananchi
jlyimo@mwananchi.co.tz

Simanjiro. Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga amefanikiwa kutatua mgogoro uliokuwepo kati ya wafugaji wa Kijiji cha Kimotorok wilayani hapa na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, kwa kuachia mifugo zaidi ya 800.

Mifugo hiyo, ikiwemo ng'ombe, mbuzi na kondoo ilikuwa imeshikiliwa na uongozi wa hifadhi ya Tarangire, baada ya wafugaji hao kudaiwa kuiingiza hifadhini kinyume na utaratibu.

Sendiga akizungumza baada ya kurejesha mifugo hiyo kwa wafugaji jana, aliwaagiza viongozi wa kata na vijiji kusimamia makubaliano na maelekezo ambayo yanapitishwa na Serikali.

"Kila vikao vikifanyika mnapaswa kuwaambia wananchi ukweli pasipo kuwaficha ili wapate uelewa juu ya maamuzi na maelekezo mbalimbali yanayotolewa, ili kuepusha migogoro isiyo na tija," alisema Sendiga.

Alitoa maelekezo kwa uongozi wa hifadhi ya Tarangire kuwaacha wafugaji waendelee kupata huduma za mifugo yao ambazo bado zinapatikana hifadhini humo, ikiwamo ya kunywea maji mifugo.

Hata hivyo, alisema ruhusa hiyo kwa wafugaji isitumike kama kigezo cha kuvunja sheria, badala yake watii taratibu na kanuni zilizowekwa na hifadhi.

Pia aliwataka wahifadhi watoe elimu zaidi na kuboresha mahusiano kati yao na wafugaji.



*Wafugaji wa Kata ya Loiborsiret, Kijiji cha Kimotorok, wilayani Simanjiro mkoani Manyara wakiswaga mifugo yao iliyokuwa imekamatwa kwa kudaiwa kuingia kwenye Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, juzi. Picha na Joseph Lyimo*

**"Kila vikao vikifanyika mnapaswa kuwaambia wananchi ukweli pasipo kuwaficha ili wapate uelewa juu ya maamuzi na maelekezo mbalimbali yanayotolewa, kuepusha migogoro isiyo na tija."** Queen Sendiga



Kwa upande wake, Diwani wa Loiborsiret, Ezekiel Lesenga (Mardadi) alimshukuru Sendiga kwa kufanikisha urejeshwaji wa mifugo yao.

Alisema wafugaji sita wa kijiji cha Kimotorok walikamatwa na ng'ombe 160, mbuzi 260 na kondoo 340 wakashikiliwa.

Alidai askari wa hifadhi waliikamata mifugo wakidai ilikuwa ikilishwa hifadhini, jambo alilodai halikuwa na ukweli wowote.

Mkazi wa Kata ya Loiborsiret, Dk Frank Oleleshwa alisema migogoro ya wananchi dhidi ya hifadhi ilikaribia kupata ufumbuzi baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuunda kamati ya mawaziri wanane wa kisekta.

Alisema mawaziri hao walifika Kimotorok ili wamshauri Rais, anaamini ilishamaliza kazi yake, kinachosubiriwa ni utekelezaji wa mapendekezo yao, ila hafahamu kinachokwamisha.

"Ninachoweza kushauri kwa sasa waliokaribu na mbunge wa Simanjir Christopher Ole Sendel wamshauri amuulize Waz ri Mkuu, Kassim Majaliw Bunge likianza swali la moj kwa moja kwa nini taarifa y kamati hiyo haijawekwa had harani, kwa nini hakuna hat ua zilizochukuliwa hadi leo,' alisema.

Mmoja kati ya wafugaji ambao mifugo yao ilikamatwa, Peter Loishiye aliiomba Serikali kuhakikisha mgogoro wao na hifadhi unamalizika na haujirudii tena.